# ATHARI NJEMA BAADA YA UTUME NO.1

<"xml encoding="UTF-8?>

BISMILAHI RAHMANI RAHIYMI

KWA JINA LA MWENYEEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

ATHARI NJEMA BAADA YA UTUME NO.1

.?Mapinduzi ya Mitume yalileta athari gani katika jamii *

BAADA YA KUBASHIRIWA UTUME

Mapinduzi ya Mitume hayakuwa bila malengo, bali yalikuwa na hadafu na madhumuni ya juhudi zilizofanywa kwa ajili ya kufikia katika malengo maalumu, nayo ni kusuluhisha jamii, na .kuwatakasa watu wa jamii nzima duniani

-:Hapana shaka kuwa Mitume imeteuliwa miongoni mwa watu, kwa kuzingatia Aya hii

لَقَدْ مَنَّ اللّهُ عَلٰي الْمُؤمِنِينَ إِذْ بَعَثَ فِيهِمْ رَسُولاً مِّنْ اَنفُسِهِمْ يَتْلُو عَلَيْهِمْ آيَاتِهِ وَيُزَكِّيهِمْ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَإِن كَانُواْ مِن قَبْلُ لَفِى ضَلالٍ مُّبِينٍ[1]

Hakika Mwenyezi Mungu amewafanyia wema mkubwa Waumini vile alivyo waletea Mtume aliye miongoni mwao wenyewe, anaye wasomea Aya zake, na anawatakasa, na anawafunza .Kitabu na hikima, ijapo kuwa kabla ya hapo walikuwa katika upotovu ulio wazi

.Maelezo kuhusiana na Aya

Hapa Mwenyeezi Mungu anawakumbusha waislamu neema kubwa aliyowapa- ya kuwaletea Mtume, na kuonyesha kuwa walikuwa katika upotevu mkubwa, na sasa wameingia katika .uongofu mkubwa mno kabisa

Lakini kwa kuthibiti kauli za Mitume katika jamii, na juhudi za viongozi wa kidini zilikuwa na athari na faida kiasi ya kwamba waliweza kuleta mabadiliko makubwa katika jamii, na athari .zao hizo zenye baraka zinaonekana katika kipindi kirefu, na zimebakia kitarekhe

Baada ya kuja Mitume, watu ambao walikuwa wakiabudu masanamu na waliopotoka na kupotea kwa kufuata sunna za kijahilia walizinduka, na hata wengine walikubali kufuata njia za

Mitume hiyo baada ya kujiona kuwa hawakuwa katika mwenendo sahihi, kama inavyosema -:Qur-ani

وَجَاء مِنْ اَقْصَي الْمَدِينَةِ رَجُلٌ يَسْعَي قَالَ يَا قَوْمِ اتَّبِعُوا الْمُرْسَلِينَ[2]

Na akaja mtu mbio kutokea upande wa mbali wa mjini, akasema: Enyi watu wangu! Wafuateni .hawa walio tumwa

Wafuateni hawa walio tumwa – yaani wafuatwe Mitume - Na vile vile kwa wale ambao * walikuwa wakitafuta uhuru wao na wamechoka na dhulma na kutokuwepo uadilifu, kwa watu madhalimu waliokuwa wametawala zama hizo, kwa kuja Mitume waliweza kupigania haki na uhuru wao. Kwa mfano;Baadhi ya watu wa Bani Israel walikubali kufuata desturi za Mtume wao, wakiwa chini ya uongozi wa - Taluti - walisimama kidete na kuwa madhubuti kwa -:kukabiliana na jeshi la – Jaluti – pale Qur-ani iliposema

فَهَزَمُوهُم بِإِذْنِ اللهِ وَقَتَلَ دَاوُودُ جَالُوتَ وَآتَاهُ اللّهُ الْمُلْكَ وَالْحِكْمَةَ وَعَلَّمَهُ مِمَّا يَشَاءُ وَلَوْلاَ دَفْعُ اللهِ النَّاسَ بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ لَّفَسَدَتِ الاَرْضُ وَلَـكِنَّ اللّهَ ذُو فَضْلٍ عَلـَي الْعَالَمِينَ[3]

Kwa idhini ya Mwenyezi Mungu waliwatimua, na Daudi akamuuwa Jaluti, na Mwenyezi Mungu akampa Daudi ufalme na hikima, na akamfundisha aliyo yapenda. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu hawapambanishi watu kwa watu basi dunia ingeli haribika. Lakini Mwenyezi Mungu ni .Mwenye fadhila juu ya walimwengu wote

Nabii Daudi alikuwa ni askari katika hilo jeshi la Mfalme Taluti. Akapigana kwa nia nzuri na* ushujaa mkubwa kabisa, hata akamuuwa mfalme wa hao maadui (makafiri), aliyekuwa akiitwa .Jaluti,basi Mwenyeezi Mungu akampa Utume na Ufalme na mengineyo kwa hayo aliyofanya

Kwa upande mwengine, kwa wale waliokuwa wamedhulumiwa wakiwa mateka chini ya viongozi hao wa kidhalimu, walipoona wamepata maficho na kujitetea kutokana na dhulma -:waliyokuwa wakifanyiwa, kwa mategemeo waliwaelekea Mitume na kuwaambia

وَمَا لَكُمْ لاَ تُقَاتِلُونَ فِى سَبِيلِ اللهِ وَالْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الرِّجَالِ وَالنِّسَاء وَالْوِلْدَانِ الَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا اَخْرِجْنَا مِنْ هَـذِهِ الْقَرْيَةِ الظَّالِمِ اَهْلُهَا وَاجْعَل لَّنَا مِن لَّدُنكَ وَلِيّاً وَاجْعَل لَّنَا مِن لَّدُنكَ نَصِيراً[4]

Na mna nini msipigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu na ya wale wanao onewa, wanaume na wanawake na watoto, ambao husema: Mola Mlezi wetu! Tutoe katika mji huu ambao watu wake ni madhaalimu, na tujaalie tuwe na mlinzi anaye toka kwako, na tujaalie tuwe na wa .kutunusuru anaye toka kwako

Baada ya kuhama Mtume Makka walisalia baadhi ya Waislamu – wanaume na wanawake na* watoto – wameadhibiwa na jamaa zao na kufungwa ndindindi, hawawezi kukimbia wakaja .Madina

Na wanadhiliwa na kutaabishwa kweli kweli, basi wanahimizwa Waislamu vikitokea vita wapigane kweli kweli na hao makafiri mpaka waweze kuwaokoa hao Waislamu .wanaotaabishwa hivyo

Basi Waislamu wa kweli wakayafuata haya, wakapigana hata wakaitia Makka mikononi mwao. Akatawalishwa liwali wa kiislamu akawatoa taabuni wale Waislamu waliokuwa wakitaabishwa .na kuomba vile, dua ilisibu baada ya amri kufuatwa

Watu baada ya kuona mafanikio katika mapinduzi waliyoyafanya Mitume waliingia katika dini ya Mwenyeezi Mungu makundi kwa makundi, kama alivyoashiriwa katika surat Nasr, pale Allah -:(s.w) aliposema

إِذَا جَاء نَصْرُ اللهِ وَالْفَتْحُ. وَرَاَيْتَ النَّاسَ يَدْخُلُونَ فِى دِينِ اللهِ اَفْوَاجاً[5]

.Itakapo kuja nusura ya Mwenyezi Mungu na ushindi

Na ukaona watu wanaingia katika Dini ya Mwenyezi Mungu kwa makundi,Natija tunayoipata katika maelezo hayo ni kwamba; kwa kuteuliwa Mitume kulisababisha harakati katika jamii, harakati ambazo ziliwafanya wale ambao waliojitakasa nafsi zao na wenye kutafuta haki kukubali kuwafuata Mitume, na kujenga umoja. Na kwa upande mwengine madhalimu walisimama kidete kukabiliana na waislamu ili kubadilisha sunna za Kiislamu walizokuja nazo Mitume,lakini kwa uweza wake Allah (s.w) hawakufanikiwa na waliyokuwa wakiyataka, - yaani kuzibadilisha sunna za Allah (s.w) - kwani ni jambo lililowazi kabisa kuwa sunna za Mwenyeezi Mungu haziwezi kubadilishwa, na Mwenyeezi Mungu siku zote huwasaidia Waumini na Waislamu kukabiliana na makafiri, kama anavyosema allah (s.w) kuelezea mafanikio ya -:Mitume

وَلَقَدْ كُذِّبَتْ رُسُلٌ مِّن قَبْلِكَ فَصَبَرُواْ عَلـي مَا كُذِّبُواْ وَاُوذُواْ حَتَّي اَتَاهُمْ نَصْرُنَا وَلاَ مُبَدِّلَ لِكَلِمَاتِ اللهِ وَلَقدْ جَاءكَ مِن نَّبَإِ الْمُرْسَلِينَ[6]

Na hakika walikanushwa Mitume wa kabla yako. Nao wakavumilia kule kukanushwa, na kuudhiwa, mpaka ilipo wafikia nusura yetu. Na hapana wa kubadilisha maneno ya Mwenyezi .Mungu. Na bila ya shaka zimekujia baadhi ya khabari za Mitume hao

Mwenyeezi Mungu huwapa Mitume yake cheo cha Utume baada ya kufahamu hali ya jamii ilivyo, na katika kipindi chote hiki cha tarekhe tumeshuhudia kuwa Mwenyeezi Mungu hatarajii lolote kutoka kwa waja wale isipokuwa baada ya kuwaongoza , kuwaonya au kuwataka wazingatie ibra kutoka umati uliopita, kwani kwa kufanya hivyo huwafanya waumini kuweza kupambanua haki na batili, na huweza kukabiliana na tabu na mashaka kutokana na fadhila na .(rehema zake Allah (s.w

وَكُـلاًّ نَّقُصُّ عَلَيْكَ مِنْ اَنبَاءِ الرُّسُلِ مَا نُثَبِّتُ بِهِ فُؤَادَكَ وَجَاءكَ فِى هَـذِهِ الْحَقُّ وَمَوْعِظَةٌ وَذِكْرَي لِلْمُؤْمِنِينَ[7]

Na yote tunayo kusimulia katika khabari za Mitume ni ya kukupa nguvu moyo wako. Na katika .haya imekujia haki na mawaidha na ukumbusho kwa Waumini

kusikia yaliyowapata wengine na natija nzuri iliyopatikana kunashajiisha moyo, ndiyo maana * Mwenyeezi Mungu akakithirisha kutaja visa vya wema na vya wabaya, tusione kuwa sisi .tumeonewa

Surat Al-Imrani aya ya 164 [1]

Surat yaasin Aya ya 20 [2]

Suratul-Baqarah Aya ya 251 [3]

Suratun –Nisaa Aya ya 75 [4]

Surat Nasr Aya ya 1-2 [5]

Surat Al-An-aam Aya ya 34 [6]

Surat Hud Aya ya 120 [7]

MWISHO